

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
**HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA**

(Barua zote zipelekwe kwa Mkurugenzi wa Jiji)

MKOA WA DODOMA

Tel.: 2354817/2321550

Fax: 2321550



Ofisi ya Mkurugenzi wa Jiji

S.L.P.1249

Dodoma

Baruapepe: [cd@dodomacc.go.tz](mailto:cd@dodomacc.go.tz)

Tarehe:01 Marchi, 2019

**TANGAZO LA ZABUNI**

**ZABUNI Na. LGA/020/2019--2020/NCS/1-10**

**ZABUNI ZA WAKALA WA UKUSANYAJI WA MAPATO KATIKA  
HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA**

1. Halmashauri ya Jiji la Dodoma inakusudia kuweka mawakala wa kukusanya Mapato kwa kupangisha maeneo mbalimbali ya kufanyia biashara kwa kipindi cha kuanzia **Julai, 2019** hadi **June, 2020**.
2. Halmashauri ya Jiji ya Dodoma inapenda kuwaalika watu binafsi, makampuni, mashirika, taasisi au vikundi vya watu vilivyosajiliwa kisheria, wenye nia na uwezo wa kuingia mikataba ya kukusanya mapato/kupangisha kutuma maombi yao kwa zabuni zifuatazo:-

<b>Na.</b>	<b>CHANZO CHA MAPATO</b>	<b>NAMBA YA ZABUNI</b>
1	Upangishaji wa banda la kuku lililoko Miyuji	<b>LGA/020/2019-2020/NCS/1</b>
2.	Upangishaji na uendeshaji wa mgahawa ulioko soko la Majengo	<b>LGA/020/2019-2020/NCS/2</b>
3.	Upangishaji wa eneo la uwekezaji wa mgahawa (zamani ghala la DODIDECO)	<b>LGA/020/2019-2020/NCS/3</b>
4.	Uendeshaji wa hudumaya choo cha kulipia kilichopo soko la Majengo	<b>LGA/020/2019-2020/NCS/4</b>
5.	Uendeshaji wa hudumaya choo cha kulipia kilichopo eneo la Nyerere Square	<b>LGA/020/2019-2020/NCS/5</b>
6.	Uendeshaji wa hudumaya choo cha kulipia kilichopo soko la Bonanza	<b>LGA/020/2019-2020/NCS/6</b>
7.	Upangishaji na uendeshaji wa mgahawa ulioko eneo la Nyerere Square A	<b>LGA/020/2019-2020/NCS/7</b>

8.	Upangishaji na uendeshaji wa mgahawa wa kuhamisha eneo la Nyerere Square B	<b>LGA/020/2019-2020/NCS/8</b>
9.	Upangishaji na uendeshaji wa machinjio ya kuku iliyoko soko la Majengo	<b>LGA/020/2019-2020/NCS/9</b>
10.	Upangishaji na uendeshaji wa bar iliyoko soko la Majengo (Pacific Bar)	<b>LGA/020/2019-2020/NCS/10</b>

3. Zabuni hii itaendeshwa katika taratibu za mfumo wa Ushindani wa Kitaifa (National Competitive Bidding) kama ilivyoelekezwa katika Kanununi za Ununuzi zilizotolewa kwa tangazo la serikali namba 446 la mwaka 2013 na marekebisho yake ya mwaka 2016 isipokuwa itakapokuwa imeandikwa vinginevyo kwenye masharti maalum ya uombaji (Bid Data Sheet).
4. Weneye nia ya kuomba zabuni hii wanaweza kupata taarifa za ziada na kukagua nyaraka za zabuni katika ofisi ya Katibu – Bodi ya Zabuni, Halmashauri ya Jiji la Dodoma Mkao Makuu, gholofa ya kwanza, chumba namba 14, S. L. P. 1249, Dodoma, kuanzia saa 1.30 asubuhi hadi saa 9.30 mchana, Jumatatu hadi Ijumaa isipokuwa siku za mapumziko ya ki-Taifa.
5. Weneye nia ya kuomba zabuni hii wanatapata **Nyaraka za Zabuni** katika lugha ya Kiswahilibaada ya kulipa ada ya **Shs. 100,000/= (shilingi laki moja tu)** ambayo haitarejeshwa (**non - refundable**). Malipo hayo yalipwe kwa **Mkurugenzi wa Jiji, Jiji la Dodoma, S. L. P. 1249, Dodoma.**
6. Mwisho wa kupokea zabuni ni tarehe **15/03/2019** saa nne (4) asubuhi, na ufunguzi utafanyika mara baada ya muda wa mwisho wa kupokea zabuni hizo mbele ya waombaji watakao amua kuhudhuria kwenye ukumbi ya mikutano ulioko jengo la Makao Makuu ya Manispaa (zamani likijulikana kama jengo la CDA), ghorofa ya pili.
7. Zabuni zote zitumwe zikiwa zimefungwa ndani ya bahasha iliyofungwa ipasavyo. Juu ya bahasha ioneshwe namba ya zabuni. Zabuni zitumwe kwa anuani ifuatayo:-  

**Mkurugenzi wa Jiji,  
Jiji la Dodoma,  
S.L.P 1249,  
DODOMA.**
8. Zabuni ambazo zitachelewa kwa muda uliopangwa na zabuni zitakazotumwa kwa barua barua pepe (e-mail) hazitapokelewa.

Tangazo hili limetolewa na:

**Ofisi ya Mkurugenzi wa Jiji,  
HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA.**